JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

"Kilimani" Iringa Road,
S.L.P. 1175,
41101 DODOMA,
Barua Pepe: rbcdodoma@pccb.go.tz.
TANZANIA.
www.pccb.go.tz

DODOMA – JULAI 1, 2019

TAARIFA KWA UMMA

MKANDARASI KUREKEBISHA MRADI WA MAJI

TAKUKURU Mkoa wa Dodoma imeingilia kati ujenzi wa Mradi wa Maji wa Kijiji cha Kelema Kuu wilayani Chemba baada ya kubaini thamani ya fedha iliyotumika kutoendana na kazi halisi iliyofanyika. Hatua hii imefanyika ikiwa ni utekelezaji wa moja ya majukumu ya TAKUKURU chini ya kifungu cha 7 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na rushwa Na. 11 ya mwaka 2007.

Katika uchunguzi wetu tulibaini thamani ya fedha haikupatikana kutokana na uwepo wa malipo zidifu ya kazi halisi zilizofanyika na kutandikwa kwa aina ya mabomba kinyume na mkataba hivyo kusababisha mradi huo kutokutoa maji. Baada ya TAKUKURU kuingilia kati, Mkandarasi wa mradi huo JUIN COMPANY LIMITED ameridhia kurekebisha mapungufu yaliyobainika na leo Julai Mosi, 2019 anaanza kazi ya kubadili mabomba na kuweka yanayostahili na pia atarejesha malipo zidifu aliyolipwa bila kustahili, hivyo jumla ya Sh. **67,542,600/=** zimeokolewa na tunatarajia wananchi watapata huduma ya maji. Mradi huo wenye thamani ya Sh. 222,978,680/= ulipaswa kukamilika tangu mwaka 2015.

Pia tumefanikiwa kumkamata Bw. GASTON MELTUS FRANCIS ambaye ni Mkurugenzi wa GLOBAL SPACE EAST AFRICA LIMITED iliyopewa kazi ya ujenzi wa kituo cha afya cha Mima wilayani Mpwapwa na ambaye tulitangaza kumtafuta Aprili 1 mwaka huu baada ya ukaguzi wetu kubaini kwamba kampuni hiyo imelipwa isivyo halali kiasi cha Sh **86,405,205/=** kwa kazi ambazo hazikufanyika katika mradi huo. Kwa sasa tunakamilisha uchunguzi wetu baada ya kumhoji Mkandarasi huyo. Aidha, TAKUKURU imefanikiwa kuokoa na kurejesha Serikalini jumla ya Sh. **11, 877,353/=** zilizolipwa kinyume na taratibu kama mshahara kwenye akaunti ya benki ya Mwalimu aliyefariki.

Pia katika robo ya Aprili hadi Juni, 2019 TAKUKURU Mkoa wa Dodoma iliendelea na majukumu yake ya kuelimisha umma, ambapo lengo kuu ni kuunganisha nguvu za jamii nzima katika mapambano dhidi ya rushwa. Tulifanya semina 28, mikutano ya hadhara 15, maonesho matatu (3) na vipindi vinne (4) vya redio.

Mkazo uliwekwa katika kuwaandaa wananchi kushiriki katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa bila kujihusisha na wala kuruhusu vitendo vya rushwa kwenye uchaguzi huo. Wananchi wameaswa kuchagua viongozi waadilifu na wanaochukia rushwa ili kuhakikisha kwamba juhudi za mapambano dhidi ya rushwa zinafanikiwa.

Pia tulishiriki katika kongamano la Siku ya Afrika ya mapambano dhidi ya rushwa ambapo Klabu ya wapinga rushwa ya wanachuo wa Chuo Kikuu cha Dodoma ilishirikishwa na kauli mbiu ilikuwa ni *kuelekea msimamo wa pamoja wa Afrika katika urejeshwaji wa mali zilizopatikana kwa njia ya rushwa.*

Aidha, tumezindua klabu 39 za wapinga rushwa katika shule na vyuo mbalimbali. Hii ni katika kujenga kizazi cha vijana ambao ni waadilifu na wanaoichukia rushwa kwani vijana ndilo jeshi kubwa hapa nchini na sehemu muhimu sana katika mafanikio ya vita dhidi ya rushwa. Tuliendelea na uimarishaji wa klabu za wapinga rushwa mpya na zilizofunguliwa siku za nyuma.

Katika robo tajwa TAKUKURU Mkoa wa Dodoma imefuatilia na kukagua miradi 34 yenye thamani ya jumla ya Sh. **32,545,418,116/=** ambapo **asilimia 95.4** ya matumizi ya fedha za miradi hiyo yalionekana kufanyika vizuri na hivyo thamani ya fedha kupatikana. Hata hivyo tumebaini viashiria vya jinai katika miradi mine (4) na hivyo tumeanzisha uchunguzi kuhusiana na uhalali wa malipo ya jumla ya Sh. **1,409,900,000/=** yaliyofanyika katika miradi hiyo. Miradi iliyokaguliwa ipo katika sekta za ujenzi wa miundombinu, afya, elimu na kilimo.

Aidha, TAKUKURU imefanya uchambuzi wa mifumo mbalimbali ya utendaji na utoaji huduma ili kubaini mianya na kushauri namna bora ya kuondokana nayo kwa lengo la kudhibiti vitendo vya rushwa. Jumla ya mifumo minne (4) ilichambuliwa katika sekta za ujenzi, manunuzi, afya na ardhi.

Kutokana na sekta ya ardhi kulalamikiwa kwa kiwango cha juu katika robo za tatu na nne za mwaka huu, tulifanya uchambuzi wa mfumo wa ufuatiliaji na utolewaji wa huduma za ardhi ambapo tayari tumekamilisha na tunatarajia mwezi huu kufanya kikao cha majadiliano na wadau ikiwemo Halmashauri ya Jiji la Dodoma ili kukubaliana namna bora ya kuondokana na mianya ya rushwa na mapungufu yaliyobainika. Hata hivyo tunawasihi wananchi kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za masuala ya ardhi ili kujiepusha na migogoro isiyo na tija na inayopoteza muda wao kuishughulikia.

Katika kipindi husika, TAKUKURU ilipokea jumla ya taarifa mia moja na thelathini na tano (135) za rushwa na makosa mengineyo ambapo tuhuma kuhusiana na Sekta ya Ardhi zilikuwa asilimia 36, zikifuatiwa na Serikali za Mitaa asilimia 31, Polisi asilimia 8, Kilimo asilimia 6 na Mahakama na Ujenzi kila moja asilimia 4. Asilimia 11 zilizosalia zilihusu Sekta za Maji, Maliasili, Afya, Madini, Ukusanyaji wa mapato na Sekta Binafsi.

Taarifa zisizohusiana na rushwa zilihamishiwa mamlaka husika na uchunguzi wa majalada nane (8) ulikamilika. Tumefungua mashauri saba (7) mahakamani yakihusisha Madiwani mawili, Mtumishi wa Kurugenzi ya Mazingira, wajumbe wa Mabaraza ya Ardhi ya Kata, Makarani wa Mahakama na watendaji wa Kata na Vijiji. Aidha mashauri mawili yalitolewa hukumu ambapo Jamhuri imeshinda shauri moja na katika shauri jingine mtuhumiwa aliachiwa huru. Mashauri thelathini (30) yanaendelea mahakamani.

TAKUKURU imejipanga kuendelea na majukumu yake katika robo ya Julai hadi Septemba, 2019 ambapo kipaumbele kitawekwa katika elimu ya kuzuia na kupambana na rushwa katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa na umuhimu wa kuchagua viongozi waadilifu na wasiojihusisha na vitendo vya rushwa. Pia tumejipanga kutumia mikusanyiko ya shughuli za mwenge wa uhuru kuwaelimisha wananchi juu ya haki na wajibu wao kuhusiana na vita dhidi ya rushwa. Pia tutafanya uchambuzi wa mifumo ya ukusanyaji wa mapato na manunuzi ya umma pamoja na kukagua miradi ya maendeleo hasa katika sekta ya elimu.

Tunawasihi wananchi wote kuendelea kutupa ushirikiano na kuwaomba wasiwe watazamaji bali washiriki kwa vitendo katika vita dhidi ya rushwa kwani hilo SI jukumu la TAKUKURU pekee bali kila mmoja ana wajibu na nafasi yake katika mapambano haya.

Aidha, tunawataka kuwa waangalifu na wasikubali kurubuniwa na 'matapeli' wanaojifanya maafisa wa TAKUKURU wanaowapigia simu na kuwatisha bali watoe taarifa mara wanapopigiwa simu au kufuatwa na watu hao. Unaweza kupiga simu ya bure namba 113 au kufika katika ofisi zetu.

Imetolewa na:

SOSTHENES KIBWENGO
MKUU WA TAKUKURU (M) DODOMA